**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA**

**MTIHANI WA UTIMILIFU MANISPAA YA SHINYANGA KIDATO CHA NNE –MEI 2023**

**023 KISWAHILI**

**MUDA: Masaa 3** ***Ijumaa, Mei 19, 2023 Asubuhi***

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali 11
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A,B na chagua maswali mawili kutoka sehemu C
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali
4. Tumia kalamu ya bluu au nyeusi
5. Andika namba ya mtihani katika kila karatasi

## SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika kipengele (i) – (x) kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kitabu chako cha kujibia

(i) Lipi ni shina la neno wameuana?

A. Wameua B. Uana C. Muuaji D. Ua E. –u-

(ii) Zifuatazo ni dhima za uundaji wa maneno mapya katika lugha isipokuwa:-

A. Kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo huchukua sura mpya kila siku
B. Kwa ajili ya kuweza kutafsiri maneno mengi kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine
C. No kupata msamiati utakaokubalika katika shughuli mahsusi kama vile benki, forodhani
D. Kwa ajili ya kuburudisha na kuonya jamii
E. Ili kukidhi hoja ya mawasiliano

(iii) Ni ufuatisho wa mawazo kutoka ubeti hadi ubeti katika shairi

A. Mizani B. Utani C. Wimbo D. Muwala E. Utoshelezi

(iv) Kifungu cha maneno ambacho hujibu maswali ya ziada kuhusu tendo katika sentensi huitwa:-

A. Tungo B. Kirai nomino C. Kiarifu D. Kirai kielezi E. Kiigizi

(v) Sentensi ipi kati ya hizi zifuatazo haina maana zaidi ya moja?

A. Kaka amefua nguo
B. Nipe sahani ya kulia
C. Suedi amenunua mbuzi
D. Eva amenunua kanga
E. Joni amempigia mpira

(vi) Kitenzi kipi kinaonesha kwamba umeme ulitoweka

A. Aliukata B. Ulikatiwa C. Ulikatika D. Tulikatiwa E. Walitakiwa

(vii) Jambo gani la msingi hupimwa katika ufahamu wa kusoma kwa sauti?

A. Uulizaji wa maswali
B. Kutamka maneno inavyotakiwa
C. Matini
D. Maswali ya kweli au sikweli
E. Majarida

(viii) Riwaya ambazo husimulia maisha ya mtu binafsi huwa katika mkondo upi?

A. Kihistoria B. Kimapenzi C. Kitawasifu D. Kiwasifu E. Kimaadili

(ix) Kiisimu upi ni mtazamo sahihi kuhusu chimbuko la Kiswahili?

A. Ngozini

B. Kiarabu
C. Shungwaya kuu
D. Pijini na krioli
E. Pwani ya Afrika Mashariki

(x) ____________ mna watu wengi

A. Aliingia B. Alipoingia C. Alikoingia D. Alivyoingia E. Alimoingia

2. Oanisha maelezo yaliyopo safu A na dhana zilizopo safu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kukamilisha maana.

| SAFU A | SAFU B |
|---|---|
| (i) Kuunda maneno kwa njia ya ubandikaji wa viambishi kabla na baada ya mzizi.<br>(ii) Neno moja huweza kubadilishwa mpangilio wake likatoa neno jingine kabisa ambapo halina uhusiano wa kimaana na lile la mwanzo<br>(iii) Maneno mawili huweza kuambatanishwa pamoja na kuunda neno moja<br>(iv) Neno linaweza kutumiwa kama aina mojawapo ya neno kisha likabadilishwa kundi la kutumia kama aina nyingine ya neno<br>(v) Kuchukua neno kutoka lugha ya kigeni na kulifanyia usanifishaji kisha kuliingiza katika lugha ya Kiswahili<br>(vi) Kufananisha tabia | A. Beberu<br>B. Kubadili kundi la neno au sifa ya neno<br>C. Kukopa maneno<br>D. Uambishaji wa maneno<br>E. Utohoaji wa maneno<br>F. Kubadili mpangilio wa fonimu (herufi)<br>G. Lami<br>H. Uambatanishaji<br>I. Ukopaji wa maneno<br>J. Mbwa mwitu |

## SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

3. (a) Taja methali unazoweza kutumia kubadilisha watu wenye tabia zifuatazo:-
   (i) Mtu mwenye tabia ya wizi
   (ii) Mtu asiyejali jeraha dogo mwilini wake
   (iii) Mtu anayerukia magari na hakubali ushauri wa katazo la anachofanya
   (iv) Mtu mwenye tabia ya kukumbatia matendo mabaya anayoyafanya mtoto wake

   (b) Bainisha virai vivumishi vinavyojitokeza katika sentensi zifuatazo kwa kuviandika katika karatasi yako ya kujibia.

   (i) Mtoto mdogo anasoma kitabu polepole
   (ii) Mwanafunzi hodari amefaulu mtihani
   (iii) Nyumba yenye wapangaji wengi imeungua moto
   (iv) Gauni jeupe lililochanika limeshonwa

(v) Agapita ni mweusi wa kuvutia

4. (a) Sentensi zifuatazo huashiria kauli mbalimbali. Bainisha kauli hizo kulingana na zinavyoieleza.
   (i) Tumeletewa muuguzi mwingine
   (ii) Kamba hukatika pembamba
   (iii) Magari yamegogana
   (iv) Anafundisha vizuri
   (v) Wanafunzi wamemsomea mgeni risala

   (b) Eleza kwa ufupi mchango wa BAKITA na TUKI katika kukua na kuenea kwa Kiswahili (Hoja mbili)

5. Bainisha miundo ya silabi katika sehemu zilizopigiwa mstari katika maneno yafuatayo:-
   (a) <u>**Ku**</u>la
   (b) Anatu<u>**i**</u>ta
   (c) Wata<u>**chi**</u>njwa
   (d) M<u>**chwa**</u>
   (e) Ame<u>**u**</u>awa
   (f) Wataku<u>**nywa**</u>

6. Bainisha aina ya makosa ya kisayansi yaliyojitokeza katika tungo zifuatazo:-
   (a) Baba amenunua kuku thaba
   (b) Juma mjini ameenda samaki kununua
   (c) Kitabu yetu amechanika
   (d) Juma amempigia mpira
   (e) Vijana serasini wamekamatwa
   (f) Nzi imeingia kwenye chai yangu
   (g) Mtoto angepelekwa hospitalini mapema angepona
   (h) Mzee Peko alichinja mbuzi zake zote
   (i) Zambi hazifai kwa mcha Mungu

7. Kwa kurumia Riwaya ya Watoto wa Mamantilie bainisha matukio matatu yanayodhihirisha hali ya umaskini kwa kuyatolea ufafanuzi.

8. Vituo vilivyobainishwa katika ramani vinahusishwa na maendeleo ya Kiswahili enzi ya utawala wa Waingereza. Unafikiri ni kwa vipi maeneo hayo yanahusika na maendeleo ya Kiswahili? (Fafanua kwa hoja sita)




**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili** kutoka sehemu hii. Swali la 10 ni la lazima

9. Mpaka sasa bado Kiswahili kinaendelea kukua na kuenea. Kwa kutumia hoja sita thibitisha ukweli wa kauli hii.
10. Ushairi wa Kiswahili kama tanzu nyingine za fasihi una kazi ya kuadilisha na kuelimisha jamii. Jadili matendo yasiyo na utu jinsi yalivyojadiliwa na wasanii katika diwani mbili ulizosoma. Tumia hoja tatu kwa kila diwani.

11. Vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa, lakini ni mara nyingi vijana hao huliangusha Taifa kwa mienendo yao. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma darasani, thibitisha ukweli wa dai hili kwa hoja tatu kutoka katika kila tamthiliya.

ORODHA YA VITABU

**Ushairi**

| | |
|---|---|
| Wasakatonge | – M.S Khatibu (DUP) |
| Malenga Wapya | - TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya Chekacheka | - T.A Mvungi (EP & D.LTD) |

**Riwaya**

| | |
|---|---|
| Takadini | - Ben J. Hanson (MBS) |
| Watoto wa Mamantilie | - E. Mbogo (HP) |
| Joka la Mdimu | - AJ Safari (HP) |

**Tamthiliya**

| | |
|---|---|
| Orodha | - Steve Reynolds (MA) |
| Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe | - E Semzaba (SEC) |
| Kilio Chetu | - Midical Aid Foundation (TPH) |